602

# THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KPSEA 2024

# KISWAHILI

## Okt. 2024 - Muda: Saa 1

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 30. Jibu maswali yote.
2. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

   02109222

   **NAMBA YAKO YA TATHMINI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
   **JINA LA SOMO**

6. Kwa kila swali 1 - 30 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku. **Hakikisha jibu lako kabla ya kuweka alama kwenye kisanduku.**
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora **KISTARI** katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano**

   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **28.** Maneno haya yanastahili kuwa katika hali ya umoja pekee. Chagua jibu lenye maneno yasiyo katika hali ya umoja.

   A yai, dirisha, chandarua
   B uso, msusi, mwiko
   C ufagio, kiti, mswaki
   D kuni, vifutio, matunda

   Jibu sahihi ni D.

   **Katika karatasi ya majibu:**

   **28.** [A] [B] [C] ~~[D]~~

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 28, kisanduku chenye herufi D ndicho kilichochorwa kistari.

9. Chora kistari chako vizuri. **KISTARI** chako **LAZIMA KIWE CHEUSI** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora **KISTARI** katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

© 2024 The Kenya National Examinations Council

**Swali la 1 hadi la 5**

*Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.*

*(Ni shuleni, saa mbili asubuhi. Tatu na Sironi wanaelekea darasani baada ya gwaride.)*

Tatu: *(Akimnyooshea mkono.)* Hujambo Sironi?
Sironi: Sijambo mwenzangu. Habari ya likizo fupi?
Tatu: *(Akitabasamu.)* __1__ rafiki yangu. Ninashukuru.
Sironi: Hongera! Nimekusikia ukiimba wimbo wa taifa vizuri na kwa ujasiri tulipokuwa tukipandisha bendera. Hata nilimwona Bwana Juma akitabasamu.
Tatu: *(Akionyesha furaha.)* Asante Sironi. Mimi hufurahia kuimba wimbo wa taifa kila mara ninapopata nafasi. Mwalimu alituambia kwamba tunapoimba wimbo wa taifa huwa tunajikumbusha historia ya nchi yetu.
Sironi: Kweli! Ni vyema kukumbuka jinsi mababu walivyoteseka wakipigania ukombozi wa nchi yetu.
Tatu: __2__ ! Hata rangi kwenye bendera ya taifa zinaonyesha mambo muhimu kuhusu nchi yetu. Kwa mfano, rangi nyekundu inasimamia damu iliyomwagika wakati wa vita vya ukombozi. Nayo rangi nyeupe inaonyesha amani.
Sironi: Nami najua kuwa kijani kibichi ni rangi **inayowakilisha** rotuba ya ardhi yetu na rangi nyeusi ni ya ngozi zetu.
Tatu: Aha! Ninafurahi kwamba unafahamu hayo.
Sironi: Ndiyo wajibu wetu haswa.
Tatu: Ninakubaliana nawe.
*(Wanakimbia kuelekea darasani.)*

**1.** Sironi alimuuliza Tatu habari ya likizo fupi. Chagua jibu sahihi ya maamkuzi kujaza **nafasi ya 1** katika mazungumzo.

A. Sina neno
B. Njema
C. Karibu sana
D. Marahaba

**2.** Sironi alimwambia Tatu kuwa ni vyema kukumbuka jinsi mababu zetu walivyoteseka wakipigania ukombozi wa nchi. Chagua jibu lenye neno ambalo Tatu angetumia katika **nafasi ya 2** kuonyesha kukubaliana na Sironi.

A. Pole
B. Jamani
C. Ajabu
D. Naam

**3.** Maneno yafuatayo yametumika katika mazungumzo kujenga uhusiano mzuri baina ya Tatu na Sironi **isipokuwa**

A. hujambo.
B. ninashukuru.
C. inasimamia.
D. ninakubaliana.

4. Tatu alimwambia Sironi kwamba wimbo wa taifa unawakumbusha historia ya nchi yao. Ni njia gani nyingine unafikiri Sironi anaweza kutumia kujikumbusha historia hiyo?

A. Kufanya utafiti mtandaoni.
B. Kutekeleza majukumu.
C. Kuheshimu watu wengine.
D. Kuhifadhi mazingira.

5. Neno, "**inayowakilisha**" limetumika katika mazungumzo. Maana yake ni

A. inayojumuisha.
B. inayohakikisha.
C. inayozingatia.
D. inayosimamia.

**Swali la 6 hadi la 9**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Tulikuwa tumetulia tuli darasani kengele ilipokirizwa ghafla. Mara, kiranja wa darasa letu akatuambia kwamba tulikuwa tunahitajika kwenye ukumbi wa shule. Bila kupoteza muda tulifululiza hadi ukumbini na kuketi. Muda si muda. Mwalimu Mkuu, aliingia.

"Hamjambo nyote?" Mwalimu Mkuu alituamkua nasi tukamjibu kwa pamoja. Aliendelea, "Habari zinazotufikia sasa ni kuwa kuna mkurupuko wa ugonjwa hatari wa kipindupindu katika kata yetu ya Upendo. Inasemekana kuwa tayari ugonjwa huu umeathiri watu wengi wakiwemo watoto wa shule. Hii ndiyo maana tumekusanyika humu ili tujifahamishe kuhusu ugonjwa huu.

Ugonjwa wa kipindupindu unaweza kusababishwa na mambo mbalimbali. Inaaminika kwamba maji machafu yakichanganyika na maji safi ya kunywa na kupikia chakula huweza kusababisha kipindupindu. Taka zinazotupwa ovyo huwa makazi ya wadudu kama vile nzi ambao husambaza ugonjwa huu. Vilevile, kutozingatia usafi wakati wa kuandaa vyakula na vinywaji kunaweza kurahisisha uenezaji wa kipindupindu.

Ni jambo la busara kuhakikisha kwamba maji machafu hayapati njia ya kuchanganyika na maji safi yanayotumiwa na binadamu. Tunastahili kuwa na mapipa au mahali maalumu pa kutupa taka na kuzichoma. Tukumbuke kudumisha usafi kila mara tunapotayarisha chakula. Aidha, tunawe mikono kwa maji safi na sabuni na kwa njia inayofaa. Naomba tushirikiane kudumisha usafi ili kujiepusha na ugonjwa wa kipindupindu. Kama tunavyojua, **kinga ni bora kuliko tiba.** Ninawatakia siku njema!"

Sote tulimpigia Mwalimu Mkuu makofi kwa hotuba yake ya kuhamasisha kisha tukafumukana.

6. Kulingana na kifungu, wanafunzi walienda ukumbini kwa sababu

A. mwalimu mkuu alikuwa amewasubiri ukumbini.
B. walikuwa wameitwa huko kuhutubiwa.
C. walitaka kumsikiliza mwalimu mkuu.
D. kiranja alikuwa amepiga kengele.

7. Mwandishi amependekeza mambo yanayoweza kufanywa ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa kipindupindu. Chagua jibu ambalo **si sahihi** kulingana na kifungu.

A. Kudumisha usafi kwa kuchoma taka.
B. Kutumia maji safi kila mara.
C. Kula chakula ambacho ni safi.
D. Kusafisha kila mahali kwa sabuni na maji.

8. Kulingana na kifungu, ni tendo lipi linaloonyesha kwamba wanafunzi wa shule hii wana heshima?

A. Wanamtii kiranja wao.
B. Wanatoka nje baada ya kusikiliza hotuba.
C. Wanakaa darasani mwao.
D. Wanamsifu Mwalimu Mkuu kwa hotuba yake.

02109222

9. Methali, "**kinga ni bora kuliko tiba,**" imetumiwa katika kifungu kumaanisha

A. tuzuie janga mapema ili tusipate hasara.
B. tushirikiane ili kukamilisha jambo kwa urahisi.
C. tufanye bidii ili tufanikiwe.
D. tuzingatie ushauri ambao tunapewa.

**Swali la 10 hadi la 12**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Hapo zamani za kale, Kondoo na Paka walikuwa wafanyakazi wa Mbwa. Kondoo na Paka walifanya kazi kwa zamu. Walisafisha nyumba, kufua nguo na kupika. Mbwa aliwalipa kila mwisho wa mwezi kwa kazi walizofanya.

Kondoo alifanya kazi yake kwa utaratibu uliofaa. Alipika chakula kitamu kama asali na kukiandaa mezani kwa njia ya kuvutia. Mbwa alifurahia kazi ya Kondoo. Paka naye alifanya kazi yake kiholela. Mara nyingi, chakula alichopika kiliungua. Chai yake ilikuwa majimaji kwa kukosa maziwa ya kutosha. Jambo hili lilikuwa likimuudhi sana Mbwa.

Siku moja, Mbwa aliamua kumchungulia Paka akipika jikoni. Alimwona akinywa maziwa. Mbwa alirudi sebuleni na kuketi akingoja Paka aandae chai. Punde si punde, Paka alileta chai mezani. Kama kawaida, Mbwa alimuuliza Paka kuhusu maziwa aliyokuwa amemwona akinywa jikoni. Paka, alikana na kuanza kulia akimlaumu Kondoo kuwa ndiye aliyemtilia fitina kwa Mbwa. Kabla ya Kondoo kujitetea, Mbwa alitoa onyo kali kwa Paka. Alimpa siku mbili pekee ajirekebishe.

Paka aliomba msamaha kwa Mbwa. Aliahidi kufanya kazi kwa bidii na kwa uaminifu. Pia, alimwomba Kondoo msamaha kwa kumlaumu bure. Mbwa na Kondoo, walimsamehe Paka wakikumbuka kwamba mwana akinyelea paja halikatwi.

10. Kulingana na aya ya kwanza,

A. Mbwa aliishi na Kondoo na Paka kwake.
B. Kondoo na Paka walifanya kazi pamoja.
C. Mbwa aliwalipa Kondoo na Paka pesa nyingi.
D. Kondoo na Paka walifanya kazi za nyumbani.

11. Uwajibikaji ni mojawapo ya maadili. Chagua jibu linaloonyesha uwajibikaji wa Mbwa katika kifungu.

A. Alipendezwa na bidii ya Kondoo.
B. Alimpa Paka nafasi ya kubadilika.
C. Alimtazama Paka akipika jikoni.
D. Alisubiri kuandaliwa chakula.

12. Kondoo na Paka walifanya kazi kwa zamu. Zamu ni hali ya

A. kusaidia wenzako katika kufanya jambo fulani.
B. kuongoza wenzako wakati wa kufanya jambo.
C. kufanya jambo na kumpisha mwingine kulifanya.
D. kufanya jambo kama lilivyofanywa na mwingine.

**Swali la 13 hadi la 15**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Kadu, Sai, Tola na Soni ni wanafunzi katika Shule ya Msingi ya Jikaze. Wote wanapenda michezo. Mwalimu wao **huwahimiza** kushiriki katika michezo mbalimbali.

Vilevile, wao husoma mtandaoni kwamba michezo hujenga misuli na kuboresha afya. Siku moja, waliamua kujadili kuhusu michezo waipendayo. Kila mmoja wao alitaja michezo inayomfurahisha. Lifuatalo ni jedwali la michezo waliyotaja.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kadu** | kwata | hoki | chesi | kandanda |
| **Sai** | voliboli | kwata | kandanda | kibe |
| **Tola** | chesi | voliboli | hoki | kwata |
| **Soni** | kandanda | chesi | kwata | hoki |

13. Kulingana na kifungu hiki, wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Jikaze wanafurahia sana mchezo gani?

A. Chesi.
B. Hoki.
C. Kandanda.
D. Kwata.

14. Kifungu hiki kinaonyesha kuwa

A. afya ya wanafunzi huimarika wakiwa shuleni.
B. vifaa vya kidijitali huwaelimisha wanafunzi kuhusu michezo.
C. wanafunzi hupenda kuzungumza kuhusu michezo.
D. mwalimu huandaa mijadala kuhusu michezo shuleni.

15. Chagua jibu lenye maana ya neno "**huwahimiza**" kama lilivyotumiwa katika kifungu.

A. Huwaashiria.
B. Huwaagiza.
C. Huwashauri.
D. Huwaongoza.

**Swali la 16 hadi la 20**

*Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16 hadi 20. Umepewa majibu **manne.** Chagua jibu lifaalo **zaidi** kati ya yale uliyopewa.*

Msimu wa mvua __16__ wakulima wengi walifurahi. __17__ kufanya kazi __18__ mashamba __19__ . Haikuchukua muda mrefu kabla ya mbegu walizopanda __20__ , yaani kuchomoza kutoka ardhini.

16. A. ulipofika
B. ilipofika
C. yalipofika
D. lilipofika

17. A. Walipiga deki
B. Walitia fora
C. Walikaza kamba
D. Walipunga hewa

18. A. baina ya
B. hadi
C. miongoni mwa
D. katika

19. A. zao
B. yao
C. kwao
D. mwao

02109222

**20.** A. kuchipuka
B. kusambaa
C. kunawiri
D. kuchanua

**Swali la 21 hadi la 30**

*Kutoka swali la 21 hadi la 30, chagua jibu sahihi.*

**21.** Chagua jibu ambalo ni umoja wa sentensi ifuatayo:

Walimu wameanza kutufundisha mada zote.

A. Walimu wameanza kunifundisha mada zote.
B. Walimu wameanza kunifundisha mada yote.
C. Mwalimu ameanza kutufundisha mada yote.
D. Mwalimu ameanza kunifundisha mada yote.

**22.** Chagua wingi wa sentensi ifuatayo:

Seremala ametumia randa kulainisha meza hii.

A. Seremala wametumia randa kulainisha meza hizi.
B. Maseremala wametumia randa kulainisha meza hizi.
C. Maseremala wametumia randa kulainisha meza hii.
D. Seremala wametumia randa kulainisha meza hii.

**23.** Pete ni pambo linalovaliwa kwenye kidole. Chagua jibu lenye pambo linalovaliwa kwenye shingo.
A. Mkufu.
B. Taji.
C. Kipuli.
D. Chupio.

**24.** Rais **alipowasili** mkutanoni, watu wote walisimama. Kinyume cha neno **alipowasili** ni:

A. alipozungumza
B. aliposhiriki
C. alipofurahi
D. alipoondoka

**25.** Halima hufanya mambo yake polepole kama kobe. Cheptoo naye ni mtulivu kama
A. bahari.
B. kaburi.
C. maji mtungini.
D. usiku wa giza.

26. Maneno yafuatayo yanafuatana vipi katika kamusi?

(i) kijiko (ii) kioski (iii) kichala
(iv) kinywa

A. (i), (iii), (iv), (ii)
B. (iii), (i), (iv), (ii)
C. (i), (iii), (ii), (iv)
D. (iii), (i), (ii), (iv)

27. Chagua jibu ambalo linaonyesha ukanusho wa sentensi ifuatayo:

Baba akipata pesa ataninunulia kitabu cha hadithi.

A. Baba hakupata pesa na hakuninunulia kitabu cha hadithi.
B. Baba asingepata pesa asingeninunulia kitabu cha hadithi.
C. Baba hajapata pesa na hajaninunulia kitabu cha hadithi.
D. Baba asipopata pesa hataninunulia kitabu cha hadithi.

28. Amon aliniandikia barua pepe nami nikamwandikia. Kwa hivyo tutasema:
A. tuliandikisha.
B. tuliandikika.
C. tuliandikiana.
D. tuliandikiwa.

29. Katana alimwoa Imani mwezi jana. Kwa hivyo tutasema Katana:

A. amepata nafuu.
B. amepata jiko.
C. amefunga nira.
D. ameshika usukani.

30. Kome ni mwekahazina wa kikundi chetu. Yeye ni mwaminifu kama njiwa. Ikiwa Choge aliibuka mshindi katika mbio za masafa mafupi, tutasema yeye ana mbio kama:

A. swara.
B. sokwe.
C. sungura.
D. simba.

02109222